

HALMASHAURI YA WILAYA YA NSIMBO

Barua pepe:info@nsimbodc.go.tz
Tovuti:www.nsimbodc.go.tz



S.L.P 688

MPANDA

Press No: NDC/ICPRU/Press no.19

27 Julai 2018

TAARIFA KWA UMMA/VYOMBO VYA HABARI

KUFUNGULIWA KWA MKUTANO MKUU WA BARAZA LA MADIWANI JULAI 27, 2018 NA MH.RAPHAEL KALINGA MWENYEKITI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA NSIMBO

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo **Mh.Raphael Kalinga** ,leo Julai 27 2018 amefungua mkutano mkuu wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa mkutano huo **Mh.Kalinga** ametoa wito kwa wataalamu wa Mipango Miji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo kuhakikisha kuwa wanaendelea kutoa elimu kwa Wananchi juu ya umuhimu wa kufanya Ujenzi kwa kuzingatia Mipango Miji badala ya kufanya shughuli za Ujenzi kiholela.

Amesema iwapo wataalam watatoa elimu na maelekezo ya kutosha yatakayoweza Wananchi kuzingatia Mipango Miji itachochea kwa sehemu kubwa ukuaji wa Miji katika Halmashauri ya Nsimbo jambo litakaloharakisha maendeleo.

Mh.Kalinga amewataka Maafisa Mipango Miji kuhakikisha kuwa Elimu inatolewa hususani kwa Wakazi wa Kata za Ibindi,na Itenka ili kuwajengea uelewa kuhusu umuhimu wa ujenzi kwa kuzingatia Mipango Miji.

Aidha **Mwenyekiti Kalinga** amewataka Wataalamu kuzingatia Kanuni Sheria na Taratibu wakati wa utoaji wa Mikataba ya kazi mbalimbali hususani za Ukusayaji wa Mapato ili kuhakikisha kuwa Wazabuni wanaopatikana wanakidhi Viwango jamo litakalo saidia kwa kiasi kikubwa kuinua mapato ya Halmashauri na hivyo kufikiwa kwa malengo mahsusi ya kuleta maendeleo kwa Wananchi.

Mwenyekiti Kalinga pia amewataka Wataalam wa Idara ya Elimu Nsimbo kusimamia kikamilifu ufundishaji mashuleni ili kuinua Kiwango cha Ufaulu katika Halmashauri. Amesema licha ya matokeo ya kuridhisha yaliyopatikana bado jitiada zaidi zinahitajika ili kuinua kiwango cha Ufaulu Nsimbo.

Kuhusu Mapambano dhidi ya UKIMWI **Mh.Kalinga** ametoa Wito kwa Wataalam na Madiwani kuwa Mabalazi katika uhamasishaji Wananchi kuunga Mkono Kampeni ya upimaji wa Virusi vya UKIMWI kwa kujitokeza kwa Wingi kupima Afya zao ili kujitambua.

Mkutano Mkuu wa Baraza la Madiwani unamalizika leo ambapo aarifa za Utekelezaji Kiidara zimewasilishwa na Kujadiliwa.

Imetolewa na :



John A. Mganga
Afisa Habari Mawasiliano na Uhusiano(W)
Kitengo cha Habari Mawasiliano TEHAMA na Uhusiano,
Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo